KIOLEZO MUHTASARI WA KITENGO CHA SHERIA CHA KITAIFA NA SHERIA ZA NCHI KUHUSU ULEMAVU

UTANGULIZI

- Watu wanaoishi na ulemavu wana haki sawa,kama mkenya yeyote yule.
- Ila watu wanaoishi na ulemavu hunyimwa haki zao mara kwa mara.
- Serikali imepitisha sheria kadhaa kulinda watu wanaoishi na ulemavu kama vile; Kitengo cha Sheria cha Watu Wanaoishi na Ulemavu cha 2003 na …
- Stakabadhi hii ina muhtasari wa sheria hizi.

HAKI MSINGI

- Watu wanaoishi na ulemavu wana haki ya kuishi.Ni kinyume cha sheria kumuua mtu anayeishi na ulemavu.
- Hakuna mtu yeyote anayeruhusiwa kubagua (kuwatendea tofauti) watu waishio na ulemavu kwa sababu ya ulemavu wao.
- Watu wanaoishi na ulemavu wana haki ya kuitwa kwa majina yao yenye heshima.

WATOTO WANAOISHI NA ULEMAVU

- Watoto wanaoishi na ulemavu wako na haki ya kupewa majina mazuri (yasiyo husiana na ulemavu wao).
- Wana haki ya kusajiliwa punde tu wanapozaliwa.
- Wana haki ya kulishwa.
- Wana haki ya kuishi nyumbani na familia zao.
- Wana haki ya kuingia sehemu za kuabudu (kanisani, Msikitini).
- Wana haki ya kucheza na rafiki zao.
- Wana haki ya kuchukua maamuzi kuhusiana na haki zao.

HAKI KORTINI

- Watoto wanaoishi na ulemavu wana haki ya kupata haki kortini.
- Panapo uhitaji, mtoto anayeishi na ulemavu ana haki ya kupata huduma za wakili bila malipo.
- Watu walio viziwi au wenye shida ya kusikia wana haki ya mtafsiri.
- Watoto wanaoishi na ulemavu hawapaswi kuhojiwa na polisi bila ya wazazi au waangalizi wao kuwepo.
- Watoto wanaoishi na ulemavu hawapaswi kufungwa jela na maaskari,na kama mtoto huyo inabidi afungwe, iwe kwa muda mfupi kabisa na atengwe kando na watu wazima.

HAKI ZA SIASA

- Watu wanaoishi na ulemavu wana haki ya kupiga kura zote.
- Watu wanaoishi na ulemavu wana haki ya kujiunga na vyama vya kisiasa.
- Watu wanaoishi na ulemavu wana haki ya kuwa wanasiasa.

USAIDIZI WA KIFEDHA

- Watu wanaoishi na ulemavu walio sajiliwa na baraza la kitaifa la watu wanaoishi na ulemavu wanaeza kupata usaidizi kutoka kwa hazina ya kitaifa ya maendeleo.
- Hazina ya kitaifa ya maendeleo inaweza kupeana msaada kwa mahitaji ya msingi kwa watu wanaoishi na ulemavu na familia zao.
- Hazina ya kitaifa ya maendeleo inaweza fadhili elimu ya watu wanaoishi na ulemavu.
- Hazina ya kitaifa ya maendeleo inaweza saidia watu wanaoishi na ulemavu kwa kuwaanzishia biashara ndogondogo.
- Mashirika yasiyokua ya serikali (NGOs) yanaweza kusaidia watu wanaoishi na ulemavu.

© Kuhenza for the Children and Kupenda for the Children 2020

NJIA ZA KUFIKIA, KUTEMBEA NA KUGEUKIA

- Majengo yanapaswa kujengwa kwa namna ambayo watu wanaoishi na ulemavu wanaeza ingia.
- Watu wanaoishi na ulemavu hawapaswi kukatazwa kuingia kwa matatu au magari yoyote ya usafiri.
- Baadhi ya watoto wanahitaji kiti cha magurudumu, mkongojo na vifaa visaidizi ili waweze kutembea.Wako na haki ya kupokea vifaa hivi kutoka kwa serikali.
- Mashirika yasiyokuwa ya serikali (NGOs), wanaeza saidia watoto kupata vifaa vya kutembelea.

MATIBABU

- Watoto wanaoishi na ulemavu wana haki ya matibabu ya dharura, daktari yeyote hapaswi kumkataza mtoto huyu matibabu hata kama mzazi hana uwezo wa kulipa.
- Baadhi ya watoto wanaoishi na ulemavu wanahitaji matibabu maalum (upasuaji, mazoezi).
- Serikali inapaswa kushughulika na mahitaji haya yote ya afya.
- Watoto wote wanaoishi na ulemavu chini ya miaka 5 wako na haki ya matibabu bila malipo.
- Madaktari hawapaswi kukataza watu wanaoishi na ulemavu huduma za afya kwa sababu ya ulemavu wao.

KAZI

- Waajiri hawapaswi kuwanyima kazi watu wanaoishi na ulemavu kwa sababu ya ulemavu wao.
- Waajiri hawapaswi kuwatendea wafanyikazi waishio na ulemavu tofauti na wale wengine.
- Watu wanaoishi na ulemavu hawapaswi kulipa ushuru wa kipato chao.

JUKUMU LA MZAZI

- Wazazi au waangalizi wana haki kwa ajili ya watoto wao wanaoishi na ulemavu.
- Wazazi au waangalizi wana wajibu kwa watoto wao wanaoishi na ulemavu.
- Baba na mama wanajukumu kwa watoto wao wanaoishi na ulemavu, hata kama hawajaoana.

WAJIBU WA MZAZI

- Wazazi wanafaa kumpa mtoto chakula cha kutosha, pahali pa kuishi, nguo, dawa, chanjo na elimu.
- Korti inaweza wafanya wazazi walipie matumizi ya mtoto.

KULINDA MTOTO KUTOKANA NA MADHARA

- Wazazi wanapaswa kulinda watoto wao kutokana na madhara (kubaguliwa, kutotunzwa, dhuluma).
- Korti inaweza fanya mzazi ambaye hamulindi mtoto wake kulipa faini ya shilingi 200,000 sawia na miaka 5 jela au zote.
- Watoto wanaoishi na ulemavu mara zengine huhitaji matunzo, kulindwa na kupedwa zaidi.

KUFICHA MTOTO ANAYEISHI NA ULEMAVU

- Watoto wanaoishi na ulemavu mara zengine huhitaji matunzo, kulindwa na kupedwa zaidi.
- Kumficha mtoto sio kumlinda.
- Korti inawezamfanya mzazi anayemficha mtoto kulipa faini ya shillingi 20,000.

ELIMU

- Watoto wanaoishi na ulemavu wana haki ya kwenda shule.
- Ni hatia kutompeleka shule mtoto anayeishi na ulemavu.
- Shule za msingi na za upili ni bure kwa wanafunzi wanaoishi na ulemavu.
- Watoto wanaoishi na ulemavu hawafai kukatazwa kusoma katika shule yeyote.

© Kuhenza for the Children and Kupenda for the Children 2020